KARMA

BARIKING MARTINEZ

WASAPU..0682838132

David alikuwa akivaa nguo baada ya kuoga Ruby avyoingia chumbani “Baby usiondoke. Lala huku bana.” Ruby alisema kwa kudeka huku akikaa juu ya kitanda. “Siwezi mpenzi. Kesho natakiwa kwenda kazini.” David alisema huku akichomekea shati. “Jamani, kesho si Jumamosi. Inamaana hutaki kufanya na mimi tena?” Ruby alisema akiamka kitandani kisha kumkubatia David kwa nyuma; David alimgeukia na kushika uso wake. “Unajua kabisa kua nataka. Basi tufanye hivi, kesho nikitoka kazini tu, ntakuja hapa moja kwa moja. Na tufanya mambo yote unayotaka tufanye. Umeskia mpenzi? Nakupenda.” David alisema kisha akachukua simu na funguo za gari lake kitandani.

“Nakupenda pia. Ntakusubiria kesho “Ruby alisema akiwa amenuna kidogo. David amuaga Ruby kwa kumbusu midomoni kisha akaondoka nyumbani kwa Ruby huku akiwasha simu yake. Wakati akipanda gari lake, alisikia meseji nyingi zikiingia kwenye simu yake. Aliweka simu yake kwenye kiti cha abiria cha mbele na kuamua kua atazisoma meseji hizo akifika nyumbani kwake. Akiwa anaendesha, meseji zilizidi kuingia kwenye simu yake na hatimaye simu yake ikaita. Alichungulia simu yake kwenye kiti na aliona ilikuwa ni mama yake Bi Eva anapiga. “Halo mama!” David alipokea simu hukuakiendelea kuendesha gari. “David, uko wapi?” Mama yake aliuliza kwa

ukali. “Nimetoka kazini naelekea nyumbani kwangu mama. Kwani kuna tatizo?” David aliuliza baada ya kuhisi mama yake hayuko sawa. “Njoo nyumbani sasa hivi. Kuna kitu cha muhimu tunahitaji kukiongelea saivi.” Bi Eva aliamuru. “Sawa mama. Nakuja sasa hivi. “David alisema kisha kukata simu. Aligeuza gari na kuanza safari kuelekea nyumbani kwa wazazi wake. Aliwaza kwa mshangao ni kitu gani muhimu hivyo mpaka mama yake kumuita nyumbani saa moja za jioni.

Hatimaye, aliwasili nyumbani kwa ya wazazi wake na kitu cha kwanza alichoona ilikuwa ni gari la Lisa imeegeshwa nje. Moyo wake ulianza kwenda mbio akijiuliza kwa mshtuko ni kitu gani Lisa amefuata kwa wazazi wake. Alitoa sauti kwenye simu yake kisha kuegesha gari lake karibu na la Lisa. Aliingia getini huku akiwa na mawazo mengi kichwani. Alivyo ingia sebuleni, alihisi damu yake kuwa baridi baada ya kuon wazazi wake na Lisa wakimsubiri. Aliwasalimia wazazi wake kwanza na kisha kumsalimu Lisa. Lisa hakuitikia na badala yake akaanza kulia. “David mwanangu, unamatatizo gani?” Mr. Edward (baba yake David) aliuliza kwa masikitiko. “Sijajua ni nini

unazungumzia baba.” David alisema huku akiketi karibu na Lisa. “Anazungumzia kuhusu wewe kumsaliti mpenzi wako. Kwahiyo kumbe kusaliti kwako ndio sababu hujataka kufunga nae ndo hadi leo eh?” Bi Eva aliuliza kwa hasira. “Unamaanisha nini kusema namsaliti Lisa? Mimi kamwe siwezi kufanya hivyo.” David alikanusha huku moyo wake ukizidi kwenda mbio na vidole vyake kuwa baridi. “Acha uongo. Nimekushuhudia kwa macho yangu mwenyewe. Kwanini unanifanyia hivyo Dave?” Lisa aliuliza huku machozi yakimbububujika mashavuni na macho yake kuwa mekundu. “Ni lini hiyo umenishughudia?” David aliuliza kwa sura yenye aibu. “Nilikuona jana.

Nilikuona wewe na yule mwandishi wa habari Ruby mkiwa mnatoka nyumbani kwako. Tena ukambusu mdomoni kabla hajaingia katika teksi iliyokua getini. “Lisa alisema huku akiendelea kulia na kufuta machozi. David alijiegemeza kwenye kochi huku akiangalia chini kwa aibu. Alinyamaza kimya kwa sababu mambo yote aliyosema Lisa ni ya ukweli. “Mwanangu, miaka mitano iliyopita ulimtambulisha Lisa kwetu. Na ukasema kwa kinywa chako mwenyewe kuwa yeye ni msichana pekee unayempenda na siku moja utamuoa. Ni nini kimetokea? Inamaana humpendi tena?” Mr. Edward aliuliza kwa mshangao. “Nampenda. Nampenda Lisa Lisa kuliko kitu chochote.” David

alisema akimgeukia Lisa na kumfuta machozi kisha kumsika mkono wake. “Naomba msamahaLisa. Sisi wanaume tunakuaga wadhaifu saingine. Nakuahidi baada ya hapa, ntamtafuta Ruby na kuachana nae kabisa. Na kabla mwaka huu kumalizika, wewe utakua mke wangu. Nakuahidi, nakuapia.” David aliomba radhi kwa Lisa. “Nitaamini vipi maneno unayosema? Ntaamini vipi kwamba hutanisaliti tena?” Lisa aliuliza kwa mashaka. “Naapa mbele yako na mbele ya wazazi wangu. Naomba uniamini.” David alisema kisha kupiga goti moja chini huku akiwa bado ameshikilia mkono wa Lisa, “Nimekuwa nikikupenda tangu siku ya kwanza tuliyo onana miaka saba iliyopita. Japokua

wakati mwingine natenda mambo ya kijinga, siku zinavyo zidi kwenda, moyo wangu ndo unavyozidi kuzama kwako. Mimi kamwe sitaki kukupoteza wewe. Lisa Paul, nakuomba uwe mke wangu." David alisema akimuangalia Lisa machoni. Bw na Bi Edward walitabasamu huku wakiwaangalia David na Lisa. "Binti yangu! Mkubalie mwanangu. Hakuna kitu kitachonipa raha zaidi kama wewe ukikubali kuwa mkwe wangu." Bibi Eva alisema akimwangalia Lisa kwa matumaini. "Tafadhali kubali kuolewa na hili toto langu jinga ili aweze kuacha wazimu na kuanzisha familia na wewe." Mr. Edward alijaribu kumshawishi Lisa. Lisa aliwangalia Bw na Bi Edward kisha

kumtazama David. Alikaa kimya kwa muda. “Ndiyo David. Ntafurahi kuwa mkeo.” Lisa alisema kwa tabasamu. David alisimama kwa furaha kisha kumnyanyua Lisa na kumbusu midomoni na kumkumbatia kwa nguvu. Bw na Bi Edward waliwafuata na wakubatia. “Haki ya Mungu baada ya mimi kuondoka hapa, ntafuata Ruby na na kumpa bonge ya buti. Na kesho asubuhi kitu cha kwanza ntakachofanya ni kwenda kununuapete nzuri ya tanzanite kwa ajili ya mchumba wangu. “David alisema na wote wakamshangilia.

Baada ya kasherehe kidogo na chakula cha jioni, David alimsindikiza Lisa nje na kumfungulia mlango wa gari yake. Alimshikilia mkono Lisa wakati anaingia kwenye gari na kumpa busu zito kisha Lisa akaondoka na gari yake. Yeye pia akaingia kwenye gari yake na kuanza safari kuelekea kwa Ruby. Alitoa simu mfukoni mwake na kukuta missed calls tatu kutoka kwa Ruby. Alliamua kumpigia simu Ruby huku akiwa bado anaendesha gari. “Mpenzi, kuna kitu nataka nikwambie lakini siwezi kukuambia kwenye simu. Nitakuambia kesho ukija kwangu baada ya kutoka kazini.” Ruby alisema mara tu baada ya kupokea simu. “Hata mimi kuna kitu nataka nikuambie. Niko njiani saivi

nakuja kwako.” David alisema kwa sauti ya kununa. “Kweli? Basi nakusubiria.” Ruby alisema kwa furaha na David akakakata simu. Dakika sita baadaye, David aliwasili nyumbani kwa Ruby. Aligonga mlango kwa nguvu na kwa haraka huku akiwaza jinsi atakavyo muacha Ruby kama alivyoahidi na kutulia na Lisa mazima. Ruby alifungua mlango akiwa na tabasamu kubwa juu ya uso mwake; David aliingia ndani ya bila kusema neno lolote. David alikaa kwenye kochi huku akiwa amekunja sura. “Ruby, kuna kitu mimi …” Ruby akamakakata kauli “Kabla hujasema chochote, uangalia pale juu ya meza” Ruby alisema akinyooshea meza kidole. David aliangalia mezani. Gafla

akatumbua macho na kuacha mdomo wazi kwa mshtuko huku akiangalia kipimo cha mimba kilichokua mezani kinacho onyesha kua mimba ipo.

TO BE CONTINUED….

David alisimama na kuchukua kipimo mezani na kukiangalia vizuri. “Una mimba?” David alimuuliza Ruby na mshtuko. “Ndiyo mpenzi. Naskia raha sana kubeba kiumbe chako ndani yangu.” Ruby alisema kwa tabasamu huku akipapasa tumbo yake. “Kwanini umefanya hivyo? Si unajua mimi nna mpenzi?” David aligomba kwa sauti kubwa. “Mimi sijui kilichotokea. Nilikua natumia vidonge vya mpango lakini naona vitakua havifanyi kazi. Mimi sijalishi kama una mpenzi. Sio lazima wewe kuwa sehemu ya maisha ya mwanangu. Naweza kumlea mwenyewe” Ruby alisema huku akikaa juu ya kochi. “Nitamueleza nini Lisa? Ataniacha mimi jamani.” David alisema

kwa kuchanganyikiwa. “Lakini mimi bado nipo. Nakupenda mpenzi wangu.” Ruby alisema akiamka kwenye kochi na kujaribu kumkumbatia David. David alimsukuma Ruby kidogo kisha akaketi kwenye kochi kubwa. “Inabidi uitoe.” David alisema huku akimuangalia Ruby ambaye alikuwa amesimama mbele yake. “Hapana. Mimi nataka kuwa na mtoto, hasa na wewe. Siwezi kutoa ujauzito wangu.” Ruby alisema huku akikaa karibu na David. “Si uliniambia ulishawahi kutoa mimba zamani? Fanya hivyo tena tafadhali! Siwezi kumpoteza Lisa.” David alimuomba Ruby. “Mimba niliyo itoa zamani, ilikua ya mwanaume nisiye mpenda. Lakini mimi nakupenda wewe sana. Naomba unisamehe lakini

siwezi kuitoa mimba hii.” Ruby alisema akisonga karibu na David. David alishika kichwa chake kwa kuchanganyikiwa. Ruby aligusa paja la David na kuanza kulipapasa taratibu. David alijiegemeza kwenye kochiakifikirini jinsi gani atamuelezea Lisa na wazazi wake. Ruby alimshika shika David kifuani; Akaketi juu ya mapaja ya David akimwangalia usoni na kujaribu kumbusu. “Hapana Ruby. Nina mawazo mengi sana kichwani.” David alisema baada ya kusogeza uso wake mbali na Ruby. “Basi acha nikusaidie kukupumzisha akili.” Ruby alisema kisha kurudisha uso wa David karibu uso wake na kuanza kumbusu. David naye akakumbusu Ruby huku ameshikilia

kiuno chake. David alimbeba Ruby na kwenda nae hadi chumbani kisha kumueka kitandani. Alipanda juu ya yake na kuanza kumpa mabusu mazito.

Mlio mkali wa simu ya Ruby simu ulimuamsha David aliekua usingizini; Ruby alipokea simu yake huku akiamka kitandani bila nguo. David aliamka na kuanza kutafuta nguo zake huku akijuta kulala na Ruby. Mwishowe alipata shati lake na kuanza kulivaa wakati Ruby akirudi chumbani. “Kuna majambazi wamevamia benki mjini. Natakiwa kuripoti kwenye habari. Na ni lazima niende sasa; mchukua video ananisubiria.” Ruby alisema akichukua taulo lake na kuingia bafuni. David alimalizia kuvaa nguo zake, huku akiwaza nini cha kufanya. Aliamua kwamba ataendelea kujaribu kumshawishi Ruby kutoa mimba; na mara tu atakapo itoa, ataachana nae

mazima. Aliondoka kwa Rubu akiwa anahisi kuchanganyikiwa na mawazo kichwani mwake. Aliendesha gari yake na kuelekea kwa Thomas huku akimpigia simu. “Tom, nnakuja kwako saivi. Nahitaji ushauri.” David alisema akiendesha gari lake. “Dave saivi ni saa saba na dakika arobaini usiku. Njoo kesho.” Thomas alikataa. “Ni kitu cha muhimu sana. Tafadhali, nisipoongea na mtu ntakua kichaa.” David alimuomba. “Sawa basi, njoo.” Thomas alimkubalia. Hatimaye David alifika kwa Thomas; alipiga honi na kijana wa kazi wa Thomas alimfungulia geti. Aliingia ndani na kuketi pamoja na Thomas sebuleni na kumuadisia yote yaliyo jiri. “David, mimi ni mshkaji wako.Na Lisa ni besti

yangu sana. Kwa jinsi nnavyo mjua Lisa, hatakubali kuendelea kuwa na wewe kabisa. Yan mtaachana mazima" Thomas alisema akiwa na uhakika. "Ndio maana nikaja kwako. Unamjua Lisa vizuri. Unakumbuka ulivyo nitambulisha kwake miaka nane iliyopita? Na sasa, nampoteza sababu ya upumbavu wangu." David alisema akuangalia chini huku akihisi kuchanganyikiwa. "Itabidi umuoe Ruby na mumlee mototo wenu." Thomas alisema akijiegemeza kwenye kochi. "Siwezi kumuoa Ruby, Nampenda Lisa. Nimekuwa pamoja naye kwa miaka saba. Japokua Ruby ni mkali kinoma. Si umeshamuonaga kwenye habari?" David alisema kwa tabasamu dogo.

“Hivi unamatatatizo gani? Unaona haya ni masiara eh? Umearibu mambo halafu unaleta matani.” Thomas alisema kwa hasira. “Najua sio utani.” David alisema kisha akalala kwenye kochi. “We, hebu ondoa viatu kabla ya kuweka miguu kwenye kochi langu.” Thomas alisema kwa kukereka. “Poa. Tulia, we nishauri cha kufanya.” David alisema huku akikaa kwenye kochi na kuvua viatu vyake. “Kitu unachoweza kufanya sasa ni kumfuata Lisa, na kumwambia ukweli. Halafu yeye ndo aamue kubaki au kuondoka.” Thomas alisema huku akinyanuka kutoka kwenye kochi. “Sidhani kama naweza kuthubutu kumwambia ukweli. Lakini naona ndo jambo nalotakiwa kufanya.” David

alisema huku akilala juu ya kochi kubwa. “Ndio kitu pekee cha kufanya. Sijui utakua unamfuata nani saa nane za usiku nikihama mkoa.” Thomas alisema huku akielekea chumbani kwake. “Sijui yani. Siamini ndani ya miezi miwili unahama mkoa” David alisema huku akiondoa vitu mfukoni mwake na kuvieka mezani. “Yap. Nimeshapata nyumba nzuri na nimepandishiwa mshahara kazini.” Thomas alisema akitoka chumbani kwake na kurudi sebuleni. “Hongera sana bro.” David alisema huku akivua shati na kulieka kwenye kochi la pembeni yake. “Asante; Chukua hili blangeti. Usiku mwema.” Thomas alisema akimkabidhi David blangeti la

kujifunikia.

Asubuhi, David aliamka kwenye kochi la Thomas. Na mara baada ya kifungua kinywa, David alikwenda kwa duka la sonara na kunua pete ya bei ghali kuliko zote yenye dhahabu nyeupe na madini ya tanzanite kwaajili ya Lisa. Alirudi nyumbani kwake na mara baada ya kuoga alimpigia Lisa simu. “Halo mpenzi wangu!” Lisa alipokea simu. “Mambo wangu, unaweza kuja nyumbani kwangu saivi?” David aliuliza kwa unyenyekevu. “Hatahivyo niko njiani nakuja kwako. Ntafika hapo sasa hivi.” Lisa alisema kisha kukata simu. Dakika chache baadaye, David kusikia honi ya gari getini kwakwe. Alikwenda kumfungulia geti Lisa. Lisa aliingiza gari yake ndani kisha akashuka kwenye gari na mifuko

mingi yenye vitu. “Baby, njoo nisaidie kubeba” Lisa alisema akiendelea kutoa mifuko kwenye gari. wakati kufanya mengi ya mboga mfuko. “Wow! Mpenzi, Ni vitu gani umenunua vingi hivi?” David aliuliza akipolea mifuko kutoka Lisa. “Ni vitu vya kupika. Nataka nikupikie leo. Mara ya mwisho mimi kuja hapa, kulikuwa hakuna kitu hata kimoja cha kupika. Wewe huendagi sokoni kabisai. “Lisa alisema huku akimalizia kuchukua mifuko kwenye gari kisha kulifunga. Moyo wa David ukaanza kwenda mbio akiwaza ni wakati gani mzuri wa kumwambia Lisa ukweli. Waliingia moja kwa moja jikoni na kuanza kueka vitu kwenye friji na kabatini. “Naona samaki, kuku na nyama. Unapika nini leo?”

David aliuliza baada ya kumaliza kupanga vitu. “Chakula cha mchana napika wali samaki. Lakini kabla sijaanza kuwa bize na kupika, kunakitu tunatakiwa tufanye kwanza.” Lisa alisema akitabasamu. “Nini hicho?” David alisema akimuangalia Lisa. Lisa alimvuta David karibu yake na kuanza kumbusu. David alitaka kumuachisha Lisa ili wasifanye chochote kabla hajamwambia kuhusu mimba lakini alijikuta akimbeba Lisa na kumueka juu ya meza ya kulia chakula. Waliendelea kubusu na kuanza kuvuana nguo.

Nusu saa baadaye, Lisa alikuwa jikoni akipika na David alikuwa amekaa sebuleni akifikiria nini kitatokea kama Lisa akikubali kuendelea na mahusiano. Alianza kufikiri kutakua na maugomvi kiasi gani kama mwanae atalelewa na Ruby na Lisa. Mawazo yalimsonga akiendelea kiwaza ‘Itakuaje kama Lisa atakuja kumchukia mwanangu kwasabu alipatikana kwa kumsaliti? Na itakua vipi mwanangu akija kumchukia Lisa kisa nilikataa kumuoa mama yake?’Mawazo yalizidi kichwani kwakwe mpaka hakuweza kuvumilia tena. Baada ya kufikiri sana, hatimaye aliona bora aachane na Lisa na kuendelea na Ruby kwa ajili ya mwanae. Alikwenda jikoni na kumkuta Lisa yuko busy akipika. “Lisa,

kuna kitu nahitaji kukuambia.” David alisema akimwangalia Lisa kwa aibu. “Niambie” Lisa alisema akiendelea kupika. David alizima jiko, kisha akamshika mkono Lisa na kumpeleka kwenye chumba cha kulia chakula. Lisa alimwangalia David kwa wasi wasi huku akikaa kwenye kiti. David na akaketi kwenye kiti kilichotazamana na cha Lisa. David alivuta pumzi kwa nguvu akifikiria ni jinsi gani atanza kuachana na Lisa.

ITAENDELEA……

David alikuwa akivaa nguo baada ya kuoga Ruby avyoingia chumbani “Baby usiondoke. Lala huku bana.” Ruby alisema kwa kudeka huku akikaa juu ya kitanda. “Siwezi mpenzi. Kesho natakiwa kwenda kazini.” David alisema huku akichomekea shati. “Jamani, kesho si Jumamosi. Inamaana hutaki kufanya na mimi tena?” Ruby alisema akiamka kitandani kisha kumkubatia David kwa nyuma; David alimgeukia na kushika uso wake. “Unajua kabisa kua nataka. Basi tufanye hivi, kesho nikitoka kazini tu, ntakuja hapa moja kwa moja. Na tufanya mambo yote unayotaka tufanye. Umeskia mpenzi? Nakupenda.” David alisema kisha akachukua simu na funguo za gari lake kitandani.

“Nakupenda pia. Ntakusubiria kesho “Ruby alisema akiwa amenuna kidogo. David amuaga Ruby kwa kumbusu midomoni kisha akaondoka nyumbani kwa Ruby huku akiwasha simu yake. Wakati akipanda gari lake, alisikia meseji nyingi zikiingia kwenye simu yake. Aliweka simu yake kwenye kiti cha abiria cha mbele na kuamua kua atazisoma meseji hizo akifika nyumbani kwake. Akiwa anaendesha, meseji zilizidi kuingia kwenye simu yake na hatimaye simu yake ikaita. Alichungulia simu yake kwenye kiti na aliona ilikuwa ni mama yake Bi Eva anapiga. “Halo mama!” David alipokea simu hukuakiendelea kuendesha gari. “David, uko wapi?” Mama yake aliuliza kwa

ukali. “Nimetoka kazini naelekea nyumbani kwangu mama. Kwani kuna tatizo?” David aliuliza baada ya kuhisi mama yake hayuko sawa. “Njoo nyumbani sasa hivi. Kuna kitu cha muhimu tunahitaji kukiongelea saivi.” Bi Eva aliamuru.  “Sawa mama. Nakuja sasa hivi. “David alisema kisha kukata simu. Aligeuza gari na kuanza safari kuelekea nyumbani kwa wazazi wake. Aliwaza kwa mshangao ni kitu gani muhimu hivyo mpaka mama yake kumuita nyumbani saa moja za jioni.

Hatimaye, aliwasili nyumbani kwa ya wazazi wake na kitu cha kwanza alichoona ilikuwa ni gari la Lisa imeegeshwa nje. Moyo wake ulianza kwenda mbio akijiuliza kwa mshtuko ni kitu gani  Lisa amefuata kwa wazazi wake. Alitoa sauti kwenye simu yake kisha kuegesha gari lake karibu na la Lisa. Aliingia getini huku akiwa na mawazo mengi kichwani. Alivyo ingia sebuleni, alihisi damu yake kuwa baridi baada ya kuon wazazi wake na Lisa wakimsubiri. Aliwasalimia wazazi wake kwanza na kisha kumsalimu Lisa. Lisa hakuitikia na badala yake akaanza kulia. “David mwanangu, unamatatizo gani?” Mr. Edward (baba yake David) aliuliza kwa masikitiko. “Sijajua  ni nini

unazungumzia baba.” David alisema huku akiketi karibu na Lisa. “Anazungumzia kuhusu wewe kumsaliti mpenzi wako. Kwahiyo kumbe kusaliti kwako ndio sababu hujataka kufunga nae ndo hadi leo eh?” Bi Eva aliuliza kwa hasira. “Unamaanisha nini kusema namsaliti Lisa? Mimi kamwe siwezi kufanya hivyo.” David alikanusha huku moyo wake ukizidi kwenda mbio na vidole vyake kuwa baridi. “Acha uongo. Nimekushuhudia kwa macho yangu mwenyewe. Kwanini unanifanyia hivyo Dave?” Lisa aliuliza huku machozi yakimbubujika mashavuni na macho yake kuwa mekundu. “Ni lini hiyo umenishughudia?” David aliuliza kwa sura yenye aibu. “Nilikuona jana.

Nilikuona wewe na yule mwandishi wa habari Ruby mkiwa mnatoka nyumbani kwako. Tena ukambusu mdomoni kabla hajaingia katika teksi iliyokua getini. “Lisa alisema huku akiendelea kulia na kufuta machozi. David alijiegemeza kwenye kochi huku akiangalia chini kwa aibu. Alinyamaza kimya kwa sababu mambo yote aliyosema Lisa ni ya ukweli. “Mwanangu, miaka mitano iliyopita ulimtambulisha Lisa kwetu. Na ukasema kwa kinywa chako mwenyewe kuwa yeye ni msichana pekee unayempenda na siku moja utamuoa. Ni nini kimetokea?  Inamaana humpendi tena?” Mr. Edward aliuliza kwa mshangao. “Nampenda. Nampenda Lisa Lisa kuliko kitu chochote.” David

alisema akimgeukia Lisa na kumfuta machozi kisha kumsika mkono wake. “Naomba msamahaLisa. Sisi wanaume tunakuaga wadhaifu saingine. Nakuahidi baada ya hapa, ntamtafuta Ruby na kuachana nae kabisa. Na kabla mwaka huu kumalizika, wewe utakua mke wangu. Nakuahidi, nakuapia.” David aliomba radhi kwa Lisa. “Nitaamini vipi maneno unayosema? Ntaamini vipi kwamba hutanisaliti tena?” Lisa aliuliza kwa mashaka. “Naapa mbele yako na mbele ya wazazi wangu. Naomba uniamini.” David alisema kisha kupiga goti moja chini huku akiwa bado ameshikilia mkono wa Lisa, “Nimekuwa nikikupenda tangu siku ya kwanza tuliyo onana miaka saba iliyopita. Japokua

wakati mwingine natenda mambo ya kijinga, siku zinavyo zidi kwenda, moyo wangu ndo unavyozidi kuzama kwako. Mimi kamwe sitaki kukupoteza wewe. Lisa Paul, nakuomba uwe mke wangu." David alisema akimuangalia Lisa machoni. Bw na Bi Edward walitabasamu huku wakiwaangalia David na Lisa. "Binti yangu! Mkubalie mwanangu. Hakuna kitu kitachonipa raha zaidi kama wewe ukikubali kuwa mkwe wangu." Bibi Eva alisema akimwangalia Lisa kwa matumaini. "Tafadhali kubali kuolewa na hili toto langu jinga ili aweze kuacha wazimu na kuanzisha familia na wewe." Mr. Edward alijaribu kumshawishi Lisa. Lisa aliwangalia Bw na Bi Edward kisha

kumtazama David. Alikaa kimya kwa muda. “Ndiyo David. Ntafurahi kuwa mkeo.” Lisa alisema kwa tabasamu. David alisimama kwa furaha kisha kumnyanyua Lisa na kumbusu midomoni na kumkumbatia kwa nguvu. Bw na Bi Edward waliwafuata na wakubatia. “Haki ya Mungu baada ya mimi kuondoka hapa, ntafuata Ruby na na kumpa bonge ya buti. Na kesho asubuhi kitu cha kwanza ntakachofanya ni kwenda kununuapete nzuri ya tanzanite kwa ajili ya mchumba wangu. “David alisema na wote wakamshangilia.

Baada ya kasherehe kidogo na chakula cha jioni, David alimsindikiza Lisa nje na kumfungulia mlango wa gari yake. Alimshikilia mkono Lisa wakati anaingia kwenye gari na kumpa busu zito kisha Lisa akaondoka na gari yake.  Yeye pia akaingia kwenye gari yake na kuanza safari kuelekea kwa Ruby. Alitoa simu mfukoni mwake na kukuta missed calls tatu kutoka kwa Ruby. Alliamua kumpigia simu Ruby huku akiwa bado anaendesha gari.  “Mpenzi, kuna kitu nataka nikwambie lakini siwezi kukuambia kwenye simu. Nitakuambia kesho ukija kwangu baada ya kutoka kazini.” Ruby alisema mara tu baada ya kupokea simu. “Hata mimi kuna kitu nataka nikuambie. Niko njiani saivi

nakuja kwako.” David alisema kwa sauti ya kununa. “Kweli? Basi nakusubiria.” Ruby alisema kwa furaha na David akakakata simu. Dakika sita baadaye, David aliwasili nyumbani kwa Ruby. Aligonga mlango kwa nguvu na kwa haraka huku akiwaza jinsi atakavyo muacha Ruby kama alivyoahidi na kutulia na Lisa mazima. Ruby alifungua mlango akiwa na tabasamu kubwa juu ya uso mwake; David aliingia ndani ya bila kusema neno lolote. David alikaa kwenye kochi huku akiwa amekunja sura. “Ruby, kuna kitu mimi …” Ruby akamakakata kauli “Kabla hujasema chochote, uangalia pale juu ya meza” Ruby alisema akinyooshea meza kidole. David aliangalia mezani. Gafla

akatumbua macho na kuacha mdomo wazi kwa mshtuko huku akiangalia kipimo cha mimba kilichokua mezani kinacho onyesha kua mimba ipo.

TO BE CONTINUED….

David alisimama na kuchukua kipimo mezani na kukiangalia vizuri. “Una mimba?” David alimuuliza Ruby na mshtuko. “Ndiyo mpenzi. Naskia raha sana kubeba kiumbe chako ndani yangu.” Ruby alisema kwa tabasamu huku akipapasa tumbo yake. “Kwanini umefanya hivyo? Si unajua mimi nna mpenzi?” David aligomba kwa sauti kubwa. “Mimi sijui kilichotokea. Nilikua natumia vidonge vya mpango lakini naona vitakua havifanyi kazi. Mimi sijalishi kama una mpenzi. Sio lazima wewe kuwa sehemu ya maisha ya mwanangu. Naweza kumlea mwenyewe” Ruby alisema huku akikaa juu ya kochi. “Nitamueleza nini Lisa? Ataniacha mimi jamani.” David alisema

kwa kuchanganyikiwa. “Lakini mimi bado nipo. Nakupenda mpenzi wangu.” Ruby alisema akiamka kwenye kochi na kujaribu kumkumbatia David. David alimsukuma Ruby kidogo kisha akaketi kwenye kochi kubwa. “Inabidi uitoe.” David alisema huku akimuangalia Ruby ambaye alikuwa amesimama mbele yake. “Hapana. Mimi nataka kuwa na mtoto, hasa na wewe. Siwezi kutoa ujauzito wangu.” Ruby alisema huku akikaa karibu na David. “Si uliniambia ulishawahi kutoa mimba zamani? Fanya hivyo tena tafadhali! Siwezi kumpoteza Lisa.” David alimuomba Ruby. “Mimba niliyo itoa zamani, ilikua ya mwanaume nisiye mpenda. Lakini mimi nakupenda wewe sana. Naomba unisamehe lakini

siwezi kuitoa mimba hii.” Ruby alisema akisonga karibu na David. David alishika kichwa chake kwa kuchanganyikiwa. Ruby aligusa paja la David na kuanza kulipapasa taratibu. David alijiegemeza kwenye kochiakifikirini jinsi gani atamuelezea Lisa na wazazi wake. Ruby alimshika shika David kifuani; Akaketi juu ya mapaja ya David akimwangalia usoni na kujaribu kumbusu. “Hapana Ruby. Nina mawazo mengi sana kichwani.” David alisema baada ya kusogeza uso wake mbali na Ruby. “Basi acha nikusaidie kukupumzisha akili.” Ruby alisema kisha kurudisha uso wa David karibu uso wake na kuanza kumbusu. David naye akakumbusu Ruby huku ameshikilia

kiuno chake. David alimbeba  Ruby na kwenda nae hadi chumbani kisha kumueka kitandani. Alipanda juu ya yake na kuanza kumpa mabusu mazito.

Mlio mkali wa simu ya Ruby simu ulimuamsha David aliekua usingizini; Ruby alipokea simu yake huku akiamka kitandani bila nguo. David aliamka na kuanza kutafuta nguo zake huku akijuta kulala na Ruby. Mwishowe alipata shati lake na kuanza kulivaa wakati Ruby akirudi chumbani. “Kuna majambazi wamevamia benki mjini. Natakiwa kuripoti kwenye habari. Na ni lazima niende sasa; mchukua video ananisubiria.” Ruby alisema akichukua taulo lake na kuingia bafuni. David alimalizia kuvaa nguo zake, huku akiwaza nini cha kufanya. Aliamua kwamba ataendelea kujaribu kumshawishi Ruby kutoa mimba; na mara tu atakapo itoa, ataachana nae

mazima. Aliondoka kwa Rubu akiwa anahisi kuchanganyikiwa na mawazo kichwani mwake. Aliendesha gari yake na kuelekea kwa Thomas huku akimpigia simu. “Tom, nnakuja kwako saivi. Nahitaji ushauri.” David alisema akiendesha gari lake. “Dave saivi ni saa saba na dakika arobaini usiku. Njoo kesho.” Thomas alikataa. “Ni kitu cha muhimu sana. Tafadhali, nisipoongea na mtu ntakua kichaa.” David alimuomba. “Sawa basi, njoo.” Thomas alimkubalia. Hatimaye David alifika kwa Thomas; alipiga honi na kijana wa kazi wa Thomas alimfungulia geti. Aliingia ndani na kuketi pamoja na Thomas sebuleni na kumuadisia yote yaliyo jiri. “David, mimi ni mshkaji wako.Na Lisa ni besti

yangu sana. Kwa jinsi nnavyo mjua Lisa, hatakubali kuendelea kuwa na wewe kabisa. Yan mtaachana mazima” Thomas alisema akiwa na uhakika. “Ndio maana nikaja kwako. Unamjua Lisa vizuri. Unakumbuka ulivyo nitambulisha kwake miaka nane iliyopita? Na sasa, nampoteza sababu ya upumbavu wangu.” David alisema akuangalia chini huku akihisi kuchanganyikiwa. “Itabidi umuoe Ruby na mumlee mototo wenu.” Thomas alisema akijiegemeza kwenye kochi. “Siwezi kumuoa Ruby, Nampenda Lisa. Nimekuwa pamoja naye kwa miaka saba. Japokua Ruby ni mkali kinoma. Si umeshamuonaga kwenye habari?” David alisema kwa tabasamu dogo.

“Hivi unamatatizo gani? Unaona haya ni masiara eh? Umearibu mambo halafu unaleta matani.” Thomas alisema kwa hasira. “Najua sio utani.” David alisema kisha akalala kwenye kochi. “We, hebu ondoa viatu kabla ya kuweka miguu kwenye kochi langu.” Thomas alisema kwa kukereka. “Poa. Tulia, we nishauri cha kufanya.” David alisema huku akikaa kwenye kochi na kuvua viatu vyake. “Kitu unachoweza kufanya sasa ni kumfuata Lisa, na kumwambia ukweli. Halafu yeye ndo aamue kubaki au kuondoka.” Thomas alisema huku akinyanuka kutoka kwenye kochi. “Sidhani kama naweza kuthubutu kumwambia ukweli. Lakini naona ndo jambo nalotakiwa kufanya.” David

alisema huku akilala juu ya kochi kubwa. “Ndio kitu pekee cha kufanya. Sijui utakua unamfuata nani saa nane za usiku nikihama mkoa.” Thomas alisema huku akielekea chumbani kwake. “Sijui yani. Siamini ndani ya miezi miwili unahama mkoa” David alisema huku akiondoa vitu mfukoni mwake na kuvieka mezani. “Yap. Nimeshapata nyumba nzuri na nimepandishiwa mshahara kazini.” Thomas alisema akitoka chumbani kwake na kurudi sebuleni. “Hongera sana bro.” David alisema huku akivua shati na kulieka kwenye kochi la pembeni yake. “Asante; Chukua hili blangeti. Usiku mwema.” Thomas alisema akimkabidhi David blangeti la

kujifunikia.

Asubuhi, David aliamka kwenye kochi la Thomas. Na mara baada ya kifungua kinywa, David alikwenda kwa duka la sonara na kunua pete ya bei ghali kuliko zote yenye dhahabu nyeupe na madini ya tanzanite kwaajili ya Lisa. Alirudi nyumbani kwake na mara baada ya kuoga alimpigia Lisa simu. “Halo mpenzi wangu!” Lisa alipokea simu. “Mambo wangu, unaweza kuja nyumbani kwangu saivi?” David aliuliza kwa unyenyekevu. “Hatahivyo niko njiani nakuja kwako. Ntafika hapo sasa hivi.” Lisa alisema kisha kukata simu. Dakika chache baadaye, David kusikia honi ya gari getini kwakwe. Alikwenda kumfungulia geti Lisa. Lisa aliingiza gari yake ndani kisha akashuka kwenye gari na mifuko

mingi yenye vitu. “Baby, njoo nisaidie kubeba” Lisa alisema akiendelea kutoa mifuko kwenye gari. wakati kufanya mengi ya mboga mfuko. “Wow! Mpenzi, Ni vitu gani umenunua vingi hivi?” David aliuliza akipolea mifuko kutoka Lisa. “Ni vitu vya kupika. Nataka nikupikie leo. Mara ya mwisho mimi kuja hapa, kulikuwa hakuna kitu hata kimoja cha kupika. Wewe huendagi sokoni kabisai. “Lisa alisema huku akimalizia kuchukua mifuko kwenye gari kisha kulifunga. Moyo wa David ukaanza kwenda mbio akiwaza ni wakati gani mzuri wa kumwambia Lisa ukweli. Waliingia moja kwa moja jikoni na kuanza kueka vitu kwenye friji na kabatini. “Naona samaki, kuku na nyama. Unapika nini leo?”

David aliuliza baada ya kumaliza kupanga vitu. “Chakula cha mchana napika wali samaki. Lakini kabla sijaanza kuwa bize na kupika, kunakitu tunatakiwa tufanye kwanza.” Lisa alisema akitabasamu. “Nini hicho?” David alisema akimuangalia Lisa. Lisa alimvuta David karibu yake na kuanza kumbusu. David alitaka kumuachisha Lisa ili wasifanye chochote kabla hajamwambia kuhusu mimba  lakini alijikuta akimbeba Lisa na kumueka juu ya meza ya kulia chakula. Waliendelea kubusu na kuanza kuvuana nguo.

Nusu saa baadaye, Lisa alikuwa jikoni akipika na David alikuwa amekaa sebuleni akifikiria nini kitatokea kama Lisa akikubali kuendelea na mahusiano. Alianza kufikiri kutakua na maugomvi kiasi gani kama mwanae atalelewa na Ruby na Lisa. Mawazo yalimsonga akiendelea kiwaza  'Itakuaje kama Lisa atakuja kumchukia mwanangu kwasabu alipatikana kwa kumsaliti? Na itakua vipi mwanangu akija kumchukia Lisa kisa nilikataa kumuoa mama yake?'Mawazo yalizidi kichwani kwakwe mpaka hakuweza kuvumilia tena.  Baada ya kufikiri sana, hatimaye aliona bora aachane na Lisa na kuendelea na Ruby kwa ajili ya mwanae. Alikwenda jikoni na kumkuta Lisa yuko busy akipika. "Lisa,

kuna kitu nahitaji kukuambia." David alisema akimwangalia Lisa kwa aibu. "Niambie" Lisa alisema akiendelea kupika. David alizima jiko, kisha akamshika mkono Lisa na kumpeleka kwenye chumba cha kulia chakula. Lisa alimwangalia David kwa wasi wasi huku akikaa kwenye kiti. David na akaketi kwenye kiti kilichotazamana na cha Lisa. David alivuta pumzi kwa nguvu akifikiria ni jinsi gani atanza kuachana na Lisa.

ITAENDELEA……

David aliwafungulia mlango wazazi wake na kuwasalimu huku akipokea mfuko kutoka kwa mama yake. “Karibuni ndani.” David alisema huku akiwaongoza wazazi wake jikoni. “Naomba utambue kuwa hatukutaka kushiriki kwenye huu ujinga.” Bi Eva alisema kwa dharau huku wakiingia jikoni. “Mama, acha hizo. Yeye ni mama wa mwanangu mtarajiwa. Nimeandaa hii sherehe ndogo kama njia ya kumpongeza. Kapandishwa cheo kuwa mtangazaji wa habari; atakua anawasomea habari kila siku usiku.” David alisema huku akifungua mfuko aliouleta Bi Eva. “Unajua sikuelewi mwanangu? Lisa alikuwa tayari kubaki na kulea mwanao kama wakwake. Na

alikuomba sana usimuache lakini bado ukampa buti. Ni nini kilikuingilia? Si ulisema mwenywe kua ulikua unampenda kwa zaidi ya miaka saba?" Mr. Edward aliuliza kwa mshangao akimwangalia David. "Baba, nilishawaambia tayari. Nimefanya hivyo kwa ajili ya mwanangu. Ingekuwa ngumu sana kumkuza mtoto katika mazingira ya aina hiyo. Mimi nataka mwanangu akue katika familia ya kawaida na ya upendo kama mimi nilivyokua." David alielezea huku akiwaongoza wazazi wake kwenye chumba cha kulia chakula. "Kuna tofauti kubwa sana mwanangu. Mimi sijawahi kumsaliti mama yako. Na nimekuwa nikimpenda tokea nilivyokuwa na miaka

17. Na sikumsubirisha kwa miaka mingi, nilimua mara tu nilivyofikisha miaka 20" Mr. Edward alieleza wakiketi kwenye viti vya chumba cha kulia chakula. "Wewe umempotezea Lisa wa watu mda. Alikueka kwenye mipango yake yote ya maisha ya baadae. Ni miezi minne tu imepita tokea muachane. Labda bado unaweza kurudiana nae." Bi Eva alisema kwa matumaini. "Mama, penda usipende ntamuoa Ruby mara baada ya mtoto kuzaliwa. Hata hivyo sijui mahali alipo Lisa. Nilishakwenda kwake mara nyingi kumwangalia anaendeleaje lakini sijampata hata mara moja. Na sasa kuna watu wengine wanaishi katika nyumba yake." David alisema akimwangalia mama yake. "Mimi najua

aliko hamia. Aliuza nyumba yake na kuhama mkoa. Nimeshaenda kumsalimia nyumbani kwake mara nyingi sana.” Bi Eva alisema kwa majidai. “Kweli? Yupo wapi? Mimi nataka kumuona tu nimjulie hali.” David aliuliza alimwangalia kwa mshangao. “Alifanya niape  kwamba sitokuambia. Ila kama utaenda kumfuata ili kurudiana nae, ntakuambia alipo.” Bi Eva alisema huku akinyanyuka kwenye kiti. “Furaha ya Lisa ndio furaha yangu. Kama anafuraha huko basi mimi nimeridhika.” David alisema na wote wakanyanyuka kwenye viti. “Huyo mpenzi wako kubuhu yuko wapi? Au haji kwenye sherehe uliyo muandalia?” Bi Eva aliuliza huku wakielekea sebuleni. “Mamaa, Ruby sio

kubuhu. Amekwenda saluni ila atarudi mda sio mrefu.” David alisema kisha wakaingia sebuleni nakujiunga na wageni waliokuja kwa ajili ya sherehe.

Dakika kumi baadaye, Ruby aliwasili nyumbani kwa David na sherehe ikaanza. Ruby aliwafuata wazazi wake David ambao walikuwa wamekaa kwenye kochi kubwa. “Shikamoo Baba David.” Ruby alimsalimia Mr. Edward kwatabasamu huku akimpa mkono. Bila kusema neno lolote Mr. Edward alimshika mkono kisha kuendelea kunya kinywaji chake. “Shikamoo mama David.” Ruby alimsalimia Bi Eva kwa tabasamu huku akimpa mkono. Bi Eva alimwangalia Ruby kwa dharau kisha akanyuka kwenye kochi na kuenda jikoni na kumuacha Ruby akiwa amenyoosha mkono. David alikuwa akizungumza na wafanyakazi wenzake Ruby. “Demu wako ni noma sana. Kitu

alichofanya kupata promosheni ni noma.” Mmoja wa wafanyakazi wenzake Ruby David. “Unamaanisha nini kusema hivyo?” David aliuliza kwa ghasia kidogo. “Kwani hujasikia? Alitiana na mkurugenzi kupanda cheo.” Mfanyakazi huyo alisema kwa kunong’oneza. “Nini? Haiwezekani. Kamwe hawezi kufanya hivyo.” “David alisema kisha kuondoka na kuelekea jikoni.

Asubuhi, David aliamka kitandani kwake pembeni ya Ruby. Alishuka kitandani taratibu ili asimuamshe Ruby; Alinyata mpaka kabatini kwake kisha akatoa pete aliyokua amenunua kwa ajili ya Lisa. Aliiangalia kwa muda kisha akanyata taratibu mpaka karibu na kitanda. Alimtazama  Ruby ambaye alikua bado amelala kisha taratibu akaupapasa uso wake. Ruby alifungua macho yake kisha alitabasamu baada ya kumuona David mbele yake. David alipiga goti moja chini akimwangalia Ruby machoni. “Ruby, nakupenda. Tena saivi nakupenda zaidi sababu umebeba kiumbe change ndani yako.Nataka ukijifungua tu, tufunge ndoa. Ruby, naomba uwe mke wangu.” David

alisema akiwa ameshikilia pete na mikono miwili. Ruby alimwangalia David bila kusema neno kisha akakaa juu ya kitanda. “David, kukaa karibu na mimi. Kuna kitu nataka nikuambie kabla sijakujibu pendekezo lako.” Ruby alisema huku akikunja miguu yake kitandani. David alikunja sura yake kidogo kisha akakaa kitandani akimwangalia Ruby. “David, nakupenda kuliko kitu chochote duniani. Kuna jambo baya nimefanya lakini naomba ujaribu kunielewa kilichonisababisha kufanya hivyo.” Ruby alisema kwa aibu. Moyo wa David ulianza kwenda mbio akikumbuka maneno aliyosema mfanyakazi mwenzake Ruby. Alianza kufikiri ni kitu gani atamfanya Ruby

kama ni kweli alilala na mkurugenzi kupata promosheni. “We niambie tu nini umefanya.” David alisema huku akiangalia kwa hasira. “Kampuni iliniambia kua nitapanda cheo mwezi na nusu uliopita. Na wakishakupandisha cheo kuwa mtangazaji wa habari, wanakueka chini ya uangalizi kwa miezi sita kukupima unavyofanya kazi. Hawakupi mkataba mpaka waone unafanya kazi vizuri ndani ya hiyo miezi sita.” Ruby alielezea akimwangalia David kwaa woga. “Sawa. Lakini bado sijaona baya ulilofanya.” David alisema kuangalia Ruby kwa makini. “Sasa, kampuni isingekubali kunipandisha cheo kama wangejua nna mimba.” Ruby alisema akimuangalia David kwa hofu.

David alisimama kutoka kitandani huku akihisi kama moyo wake unataka kutoka nje ya kifua. “Ni kitugani unataka kuniambia?” Davidaliulizakwa hasira. “Naomba unisamehe David. Lakini ilinibidi nitoe mimba. Kampuni kamwe haiwezi kukubali mwanamke mjamzito asome habari.” Ruby alisema kwa uoga huku macho yake yakilenga lenga machozi. “NINI? OH MY GOD!” David alisema kwa kupanick. “Umeniulia mwanangu? Unawezaje kufanya kitu kiovu kama hicho? Kisa promosheni.Unajua ni mangapi nimepitia kwa ajili yako? Unajua nimeumia kiasi gani kumuacha kipenzi change Lisa kisa hiyo mimba?” David aliuliza kwa nguvu na kwa hasira huku

mishipa ikimtoka kichwani kwake. “Mimi bado nakupenda mpenzi wangu. Na mimi bado nipo, tunaweza tengeneza watoto wengine kibao mme wangu.” Ruby alisema huku akishuka kitandani na kumfuata David.

Machozi yalianza kumtoka David na mawazo yalimsonga. Aliwaza mambo yote aliyo haribu kwa ajili ya Ruby. Alikumbuka jinsi Lisa alivyomlilia akimuomba asimuache; jinsi Lisa alikuwa tayari kumpokea mwanae kama wakwake. Alimtazama Ruby aliyekua amesimama mbele yake na kumuwasha kibao cha nguvu usoni; Ruby akaanguka juu ya kitanda na kuanza kulia. David aliondoka chumbani kwa sekunde kadhaa kisha akarudi akiwa ameshikilia panga na kunyooshea Ruby ambaye alikuwa amekaa juu ya kitanda. “Sasa, kama unathamini maisha yako, utanijibu ukweli, je ulitiana na mkurugenzi kupanda cheo?” David aliuliza huku machozi yakimshuka

mashavuni. “Ndiyo. Ilibidi niwe na mahusiano na mkurugenzi kupanda cheo.” Ruby alisema huku akilia. “Ruby, nnakupa sekunde 10 uondoke nyumbani kwangu.mba yangu. Naapa kwa jina la Mungu, nitakukata koromeo kama ukiwa hapa bado.” David alisema kwa hasira. “Naomba angalau nivae nguo zangu.” Ruby aliuliza sababu alikua amevaa chupi na brazia tu. “10 … 9 … 8 …” David alianza kuhesabu. Ruby alikimbia nje kwa mbio zake zote.

David alichukua simu yake na kujaribu kumpigia Lisa lakini simu yake ilikuwa haipatikani. Alichukua suruali ya jeans na t-shirt kabatini na kuzivaa haraka haraka. Alimpigia simu mama yake huku akichukua funguo za gari lake na kuelekea nje. “Mama, naomba uniambie anapoishia Lisa. Tafadhali nahitaji kuonana nae.” David alimuomba mama yake huku akifungua geti lake. “Nimeshakwabia, aliniapisha nisikeambie alipo.” Bi Eva alisema huku David akikimbia gari lake na kuliwasha. “Wewe ulisema jana kama nataka kurudiana nae ndio utaniambia anapoishi saivi.” David alisema akiendesha gari na kulipaki nje; kisha alishuka na kuacha mlango wa gari

wazi. “Kweli? Unaenda kurudiana nae? Safi sana. Hata haishi mbali. Ni mkoa wa karibu tu, tena nyumba anayo ishi, inaangaliana na hoteli flani maarufu sana.” Bi Eva alimuelezea David akiwa anafunga geti lake kisha akarudi ndani ya gari. “Sawa mama, we niambie ni wapi tu.” David alisema na kuanza kuendesha gari. “Ntakutumia meseji mda sio mrefu.” Bi Eva alisema kisha David akakata simu. Dakika chahe baadaye, David kupokea meseji kutoka kwa mama yake. Na mara baada ya kuisoma aliendesha gari yake kwa mwendo wa kasi sana.

Masaa mawili baadaye, David aliwasili katika anwani mama yake aliyompa. Alishangaa kuona nyumba nzuri kubwa mpaka akadhani labda alikua amekosea njia kwa sababu hakufikiri Lisa anauwezo wa kuishi kwenye nyumba hama hiyo. Alipaki gari yake kisha kugonga geti. Mlinzi wa getini alifungua na David akamuulizia Lisa. Mlinzi alimuonyesha David mlango wa kuingia ndani na kumwambia aende kuugonga. David aligonga mlango akiwaza maneno atakayo muambia Lisa ili aweze kukubali kurudiana nae. Baada ya mlango kufunguliwa, David alibaki mdomo wazi kumuona Thomas kasimama mbele yake kifua wazi. “Thomas? Unafanya nini huku?” David

aliuliza kwa mshangao. “Unamaanisha nini kuuliza hivyo? Hii ni nyumba yangu, karibu ndani.” Thomas alisema kisha David aliingia ndani. Thomas alimuongoza David mpaka sebuleni na kukaa pamoja; David alibaki alishangaa uzuri wa hiyo nyumba. “Mimi nimekuja hapa kumtafuta Li …” David hakuweza kumaliza sentesi yake kwa sababu alimuona Lisa anakuja sebuleni akiwa amevaa kanga tu kifuani. Lisa alienda moja kwa moja kwa Thomas kisha akaketi kwenye mapaja yake. “Hee! Nini kinaendelea hapa?” David aliuliza kwa fujo. “David, nimekuwa nikimpenda Lisa kabla hata yaw ewe kumjua. Sema nilikua domo zege sana kipindi kile kumwambia kuhusu hiai zangu. Nilikua

nikisubiria muachane ili niweze kumwambia lakini miaka ilipita na Lisa alishindwa kukuacha japokua ulikua ukimfanyia mambo ya upuuzi sana. Nilikata tamaa lakini wewe ulivyo amua kumuacha, nilipata ujasiri wa kumwambia ukweli na hatimaye sasa ni wangu. Na kamwe siwezi kumuacha." Thomas alielezea kwa tabasamu. "Haiwezekani. Lazima utakua unanitania." David alisema kwa mshangao. "Lisa tafadhali, kama umefanya hivi kunikomesha, naomba tu uache mpenzi. Kama ni adhabu, naomba unitafutie adhabu nyingine. Nakupenda sana Lisa." David alimuomba Lisa. "Hapana David. Hatutakaa turudiane kamwe.

Nilivyomuonaga Tom kwa mara ya kwanza, nilimpenda lakini sikudhani kama alinipenda pia. Laiti ningejua kama alikua ananipenda, Mungu anajua tungekua wapi sasa. Unaona hii?"  Lisa aliuliza akimuonyesha David mkono wake. David alipigwa na butwaa kuona pete ya uchumba kidoleni mwa Lisa. "Ati nini?" David aliuliza akisimama kwa hasira. "Ndiyo David, miezi mitano ijayo, Lisa ni atakuja kuwa Mrs. Thomas." Thomas alisema akitabasamu kisha Lisa akamgeukia na kumpa busu zito. David akawatazama kwa hasira kisha akapiga teke kwenye meza ya kioo ya sebuleni kwa nguvu mpaka akavunja kioo. "David, ondoka nyumbani kwetu kabla sijakuitia polisi." Thomas alisema

huku akizungusha mikono yake kiunoni mwa Lisa. David aliwaangalia Lisa na Thomas kwa hasira kisha akaondoka kwenye nyumba yao huku bado hakuweza kuamini kilichotokea.

-MWISHO-